## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

### Awamu ya 1    Mwaka wa 1

# 51 Merikebu (meli) ya Paulo inavunjika

## Marejeo

Matendo ya Mitume 27; 2 Wakorintho 11:23-28; Marko 16:16

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba lazima tumtii Mungu kwa njia zote. Hii itatuletea wokovu

## Maneno maalum

1. Paulo + mfungwa + Feliki + Agripa + Kaisari
2. Italia + meli + shida + kimbilio + Bandari nzuri + Foinike + kaa baridi.
3. Hatari + kutosikiliza + upepo kidogo + tufani ( dhoruba) + tupa baharini + hakuna mwezi + hakuna jua + hakuna tumaini.
4. Paulo + changamka + uhakika + Mungu alinda
5. Usiku 14 + ardhi + tupa nanga + kaa melini
6. Kucha (pabauka) + kula + kisiwa + mawimbi +ukingo + okoka wote
7. Utii (usikivu) + Mungu atumisha usalama + tusaidie + tuongoze

## Maswali

1. Paulo alipoenda mahakamani aliwambia nini?
2. Mbona Paulo alitakiwa aende Rumi?
3. Alifikaje kule?
4. Mbona ilikuwa hatari kusafiri?
5. Meli iliyumbishwa na dhoruba, Paulo aliwambia watu waliokuwa kwa meli eti nini?
6. Paulo alijuaje chenye kitatokea?
7. Dhoruba ilikuwakopo kwa muda gani?
8. Mbona Paulo alipaza sauti, “Msipobaki wote kwa meli hatutaokoka?”
9. Hawakukuwa wamekula kwa muda gani?
10. Watu wangapi waliokoka?
11. Waliendaje kutoka kwa meli mpaka kwa kisiwa?
12. Lazima tufanye nini ili tuokoke?


## Majibu

1. Aliwambia hasa alichoamini.
2. Alitaka ahukumiwe na Kaisari Augusto.
3. Kwa meli
4. Ilikuwa wakati mbaya ya kusafiri kwa ajili ya hali ya anga.
5. Mungenisikiliza hamngeweza safari, sasa changamkeni. Hakuna atakayeumia wala kufa.
6. Mungu alikuwa amemwambia kwa maono.
7. Siku kumi na nne na usiku.
8. Watu walikuwa wameteremsha mashua ndogo ili watoroke.
9. Siku kumi na nne
10. Watu 276.
11. Baadhi yao waliogelea na wengine walijishikilia kwa mbao zilizofunjika kwa meli.
12. Lazima tuelewe, tuamini na tutii Mungu.

**51.1** Paulo na mitume walisafiri mwendo mrefu wakieneza habari ya injili. Paulo alitaabika kwa njia nyingi akitumikia Mungu, hata sasa alichukuliwa kama mfungwa. Alihukumiwa na mafarisayo, Liwali Feliki Mrumi na mfalme Agripa. Baadaye Paulo aliuliza aende ahukumiwe na Kaisari Augusto huko Rumi katika Italia.

Wakati wote Paulo aliambia mahakama sawia na anavyo amini. Aliwambia vile Mungu alimchagua eneza habari ya injili. Aliwambia vile Yesu alikufa na akafufuka. Mfalme Agripa alisema, "Umekuwa karibu sana kunishawishi niwe Mkristo!"

**51.2** Ili afike Italia, sharti asafiri kwa meli. Wakati haukukuwa mzuri wa kwenda kwa maji. Safari ilikuwa na shida. Meli ilikimbilia bandari nyingi ikitafuta usalama. Ikaweka nanga kwa bandari iitwayo Bandari nzuri kwa kisiwa cha krete. Walifikiri labda wangejaribu wafike bandari kubwa ya Foinike kule Krete na wakae huko wakati wote wa baridi.



**51.3** Meli ilikuwa imebeba watu 276 pamoja na mizigo ya nafaka. Paulo alijua kuwa kutakuwa na hatari kwa kila mtu aliyeko melini. Hakuna aliyemzikiliza. Mwanzoni meli ilipoondoka bandarini, upepo ulivuma kidogo kidogo. Baadaye upepo uitwao Eurakilo ulianza kuvuma na dhoruba ikafwata.

Meli ilielekezwa kwa kisiwa kidogo cha Kauda. Kusaidia meli isigwame ndani ya mchanga, walituba mizigo na vyombo ndani ya bahari.


Dhoruba iliendelea kuwa mbaya na meli ilielekezwa katikati ya bahari. Hawakuona mwezi. Hawakuona jua, Hawakujua wako wapi. Wote hawakukuwa na tumaini ya kuokoka.

**51.4** Paulo alichukuwa jugumu na kusema. "Mungenisikiliza hamngeanza safari, lakini changamkeni mkule hakuna atakaye umia au kufa." Mbona Paulo alikuwa na uhakika? Mungu alikuwa amemwambia kwa maono. Mungu atamlinda yeye na kila mtu alioko kwa meli. "Akawaambia tutaelekezwa tuende kwa kisiwa ndogo."

**51.5** Kufika usiku wa kumi na nne walihisi kwamba wako karibu na ardhi. Wakapima kwenda chini ya maji ilikuwa pima 20 tena pima 15 wakateremsha nanga nne. Hawakutaka kupiga mwamba. Watu waliteremsha mashua ndogo ili watoroke. Paulo alipaza sauti, "Msipobaki wote kwa meli hatutaokoka." Walifanya vile Mungu alitaka.

**51.6** Wote walingoja kukapambauka. Paulo akaamuru tena. "Lazima wote mkule, mpate nguvu kwa sababu kwa siku kumi na nne hamjakula." Paulo alishukuru kwa ajili ya chakula mbele ya kila mtu. Wakaanza kula.

Nafaka ilitupwa tena baharini kulipopambauka, walitoa nanga, meli ikaelekezwa kwa kisiwa. Iligwama na mawimbi makubwa yakavunja mgongo wa meli. Maaskari wa Rumi walitaka kuwaua wafungwa. "Hapana." Akida alikataza. Watu wote walifika ukingoni kwa kuogelea au kujishikilia kwa mbao zilizofunjika kwa meli. Wote waliokoka.



**51.7** Kwa ajili ya kutii maagizo ya Mungu, wote waliokoka. Hii inatufundisha kwamba tukitii, tuamini na tuelewe tunaweza kuokoka.

Mungu huwa anatuweka salama kwa maisha yetu, "Usitutie katika majaribu. Tuokoe na maovu." Mungu anatwambia kwamba kwa njia ya Yesu, Mwanawe tunatumaini la uzima wa milele. Tujifunze kutii amri zake. Tunaomba Mungu atusaindie na atuongoze.